Ministère des Affaires Sociales

# KUSOMA NA KUANDIKA

## Buku ya mwanafunzi

CRS

KISWAHILI


2



Edition 2018

# KUSOMA NA KUANDIKA

## Buku ya mwanafunzi



# YALIYOMO

**UTANGULIZI** ........................................................................ 1
**INGILIO** ........................................................................ 2

**KIPINDI CA 1 : KUISHI VIZURI NAFASI YAKO**

**Juma ya 1** : Kijiji ........................................................................ 4
**Juma ya 2** : Mji ........................................................................ 8
**Juma ya 3** : Ndoa ........................................................................ 12
**Juma ya 4** : Sherehe ya ceti ........................................................................ 16
**Juma ya 5** : Usafi wa mwili - Usafi wa nguo na cumba ........................................ 20
**Juma ya 6** : Matunzo - Vituo vya afya ........................................................ 24

**KIPINDI CA 2 : KUKINGA MAZINGIRA**

**Juma ya 8** : Cakula ........................................................................ 30
**Juma ya 9** : Matunda ........................................................................ 34
**Juma ya 10** : Mimea - Mavuno ........................................................................ 38
**Juma ya 11** : Kukinga mazingira ........................................................................ 42
**Juma ya 12** : Nyama za ufugo ........................................................................ 46
**Juma ya 13** : Nyama za pori ........................................................................ 50

**KIPINDI CA 3 : KUENDELESHA JIMBO MBELE**

**Juma ya 15** : Kazi ya shamba ........................................................................ 56
**Juma ya 16** : Kazi ya mikono ........................................................................ 60
**Juma ya 17** : Uongozi ........................................................................ 64
**Juma ya 18** : Barabara - wanda - jito ........................................................ 68
**Juma ya 19** : Vyombo vya usafiri ........................................................................ 72
**Juma ya 20 :** Gari lla mabawa ........................................................................ 76
**Juma ya 21** : Micezo za kiasili ........................................................................ 80
**Juma ya 22** : Micezo za kikundi ........................................................................ 84
**Juma ya 23** : Micezo za kipekee ........................................................................ 88

## UTANGULIZI

Kama ilivyo andikwa katika utangulizi wa mpango wa taifa unao husika na kuwarudisha shule la msingi waliokosa bahati hiyo nchini Jamuhuri ya Kidemokratia ya Kongo, elimu ya kitaifa ina lengo la kumfanya mkongomani awe raia mwenye kujifalia mwenyewe na kufalia jamii, paoja na kumuwezesha kukuza maendeleo ya nchi na utamaduni wa kitaifa (Mfumo wa Sheria N° 14/004/ wa tarehe 11/12/2004 ya Elimu ya Kitaifa).

Ili kufikia lengo hili, baada ya mpango huu inatakiwa mtoto mkongomani yeyote awe na uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu ; kuelewa na kujieleza katika lugha ya taifa na ya kifaransa. Kwa hiyo, mpango wa kuwarudisha watoto shuleni ni bahati ya pili ambayo yasaidia watoto wakongomani kujiingiza katika ulimwengu wa kazi na kujiundia hivi ujio nzuri.

Hata hivyo, kwa sababu ya machafuko mbalimbali ambayo nchi imeshuhudia katika miaka iliyopita, ni wazi kwamba ubora wa elimu kwa jumla, na wa mpango ya kuwarudisha watoto shuleni kwa njia ya pekee, unaendelea kuharibika miaka baada ya miaka. Hali hii inaonekana hasa katika kusoma na kuandika. Mashindano mbalimbali ya taifa (TENAFEP) zinaonyesha kwamba wanafunzi wamoja wanaomaliza viwango vitatu vya urudishaji shuleni wana matatizo ya kusoma na kuandika vizuri pamoja na kuelewa wanayo isoma.

Kwa kukabiliana na matatizo haya, Wizara wa Mambo ya Kijamii imekamata hatua zinazolenga kuboresha elimu isiyo rasmi. Hatua hizi zimeingizwa katika mbinu kubwa ya sekta ya elimu na mafunzo, ambayo kutoa vitabu vya kusoma na kuandika ni sehemu tu.

Nashukuru mashirika USAID na UKAID ambazo, kupitia mradi ACCELERE, zimetupa msaada wa kiufundi na kipesa kwa ajili ya uandishi wa kitabu hiki.

Mradi ACCELERE, ambao mbinu yake ya mafunzo inayoleta maendeleo kwa kuunganisha sauti za herufi, kusoma na kuelewa maandiko, unaleta matumaini ya kuyamaliza matatizo ya shule la kusoma na kuandika.

Kwa hiyo, nawaalika waalimu, ambao ndio watumizi wa kwanza wa kitabu hiki cha mafunzo, wakitumie kwa faida ya wanafunzi.

**Eugène SERUFULI NGAYABASEKA**

Waziri wa Mambo ya Kijamii

# INTRODUCTION

Répondant à une dynamique régionale et internationale et se basant sur des standards mondialement établis avec une vue sur nos réalités, le Ministère de l'Enseignement Primaire, Secondaire et Professionnel a élevé les sous-branches lecture et écriture au rang de branche à part entière.

En vue d'améliorer la qualité des enseignements-apprentissages de cette discipline transversale dans les Centres de Ratrapage Scolaire, le Ministère des Affaires Sociales met à la disposition de l'apprenant et de l'éducateur un matériel didactique en conformité avec le programme national.
Au niveau 1, la langue congolaise est à la fois langue d'enseignement et branche enseignée. Le français n'est, à ce niveau, qu'une branche enseignée. Son apprentissage est limité à l'oral.

C'est précisément au niveau 2 que les acquis en langue congolaise sont transférés au français. Dès lors que les mécanismes de base du décodage sont installés dans une langue familière, les apprenants devraient aller plus sûrement et plus vite en français.

L'élaboration du manuel et du cahier de lecture de l'apprenant accompagnés du guide de l'éducateur (trice) se fonde sur les découvertes scientifiques les plus récentes, bien éprouvées et tout à fait fiables.


Dans la progression des enseignements-apprentissages, le noyau de base reste l'unité d'apprentissage. Elle correspond à une semaine d'enseignement-apprentissage qui exploite un sous-thème et se répartit en six séances en français et quatre en langue congolaise. La première est consacrée à la compréhension d'un message oral et la dernière à la consolidation des acquis de la semaine suivie d'une production écrite.

Ce cahier de lecture complète le manuel. C'est un merveilleux outil conçu pour approfondir les types d'exercices écrits et oraux faits en classe. Nous invitons les éducateurs / éducatrices ainsi que les parents d'apprenants à accompagner et encourager les apprenants à s'approprier le contenu de ce matériel didactique, riche en activités de lecture et d'écriture, et qui, sans aucun doute, leur permettra d'acquérir les compétences escomptées dans ce domaine.

## KIPINDI CA KWANZA

# KUISHI VIZURI NAFASI YAKO

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora kijiji cangu.

## Nasoma herufi.

a k d j m i n sh mb

A K D J M I N Sh Mb

a k d j m i n sh mb

A K D J M I Sh Mb

## Natunga matamko.

| | | |
|---|---|---|
| k | a | sh |
| n | i | d |
| m | j | mb |

Sha

....................

....................

....................

## Natunga maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ja | mba | na |
| ji | ki | mi |
| da | sha | |

shamba

....................

....................

....................

## Natunga misemwa.


| | |
|---|---|
| imba | mama |
| shamba | lala |
| kijana | ana |
| maji | kamba |

Kijana ana shamba.

......................................

......................................

Natazama.



Nasoma.

## Kijiji Kidima

Dani anaishi kijiji Kidima.

Aisha anaishi kijiji Kidima.

Dani na Aisha ni kaka na dada.

Jamaa ina makao na shamba Kidima.

Kijijini Kidima, jamaa inakaa daima.

Najaza misemwa hii na maneno yanayokosa.

1. Jamaa ina ………… na shamba ……………
2. Dani na Aisha ni ……. na dada.

Nasoma herufi, matamko, maneno na misemwa.

a k d j m i n sh mb
Sh A K M J I N D Mb
*mb j k d m i a n sh*
*I A M D J K Sh Mb*

Ja ka sha mba di ja ni ma

dini Shamba maisha daima kamba mamba
kaka dada jina jana

Mama anaimba.

Kaka anaimba.

Dada ni kijana.


Mamba inaishi majini.

---

Najaza misemwa hii na maneno yanayokosa.

1. Aisha ............kijiji kidima.
2. Jamaa inakaa ................

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora barabara nene.

## Nasoma herufi.

b e u l c o nd ng mw
B E U L C O Nd Ng Mw
*b e u l c o nd ng mw*
*B E U L C O Nd Ng Mw*

## Natunga matamko.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | o | c | ng | n | l |
| nd | sh | u | e | k | a |
| b | d | mw | j | mb | i |

ngo

.....................

.....................

.....................

## Natunga maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| be | du | ndo | mwa |
| nde | ngu | ka | shu |
| ba | na | lu | |

mwaka

.....................

.....................

.....................

## Natunga misemwa.

| | | |
|---|---|---|
| ndoa | nguo | lunga |
| mwaka | duka | kesho |
| mlango | kula | |
| enda | ingia | |

Lunga ndoa mwaka kesho

.........................................

.........................................

Natazama.



Nasoma.

Mji Kenga

Dani anaenda mjini Kenga.

Mji  Kenga una mitaa mitatu.

Katika kila mtaa, kuna makao mengi.

Kila mwaka, jamaa inalima shamba.

Katika mji Kenga kuna amani.

Natengeneza msemwa huu.

mtaa, kila katika mengi makao kuna. ...................................

..............

Nasoma herufi, matamko, maneno na misemwa.

b e u l c o nd ng mw B E U L C O
Nd Ng Mw *b e u l c o nd ng*
*mw B E U L C O Nd Ng Mw* a
k d j m i n sh mb Sh A K M
J I N D Mb *mb j n k d m i a n*
*sh I A M D J K Sh Mb*

Ndu nge lo bi Mwe mbu ko ndo

Udongo ndoa mwaka duka ishi buku kuku
mwendo kijiko mbilika

Mbu inaniuma.

Shabani analunga ndoa leo.

Baba anaenda shambani.

Mama ananunua shuka mbili.


---

Natengeneza msemwa huu.

amani Katika Kenga mji kuna.

.......................................

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora zawadi moja.

## Nasoma herufi.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | h | s | y | f | z | ngw | ch | nz |
| W | H | S | Y | F | Z | Ngw | Ch | Nz |
| w | h | s | y | f | z | ngw | ch | nz |
| W | H | S | Y | F | Z | Ngw | Ch | Nz |

## Natunga matamko.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| m | o | c | | ng | l | nz |
| nd | sh | u | e | k | a | ch |
| b | d | n | j | mb | i | ngw |
| w | h | s | y | f | z | mw |

fe

....................

....................

....................

## Natunga maneno.

| | | |
|---|---|---|
| fe | chi | hu |
| wa | si | zi |
| ngwa | nda | ka |

wazi

....................

....................

....................

## Natunga misemwa.

| | | |
|---|---|---|
| feza | sisi | hewa |
| ziwa | sifa | owa |
| feza | ndugu | |

Feza na Sifa ni wandugu.

.......................................

.......................................

Natazama.



Nasoma.

Siku kuu

Leo ni siku kuu ya ndoa.

Ndoa ya Safi na Chunza.

Bibi na bwana wana kiceko midomoni.

Waalikwa wanafika na zawadi zao.

Zawadi hizo : cungwa na nguo.

Katika msemwa « Zawadi hizo : cungwa na nguo. », natia maneno mengine nafasi ya « cungwa, nguo ».

Zawadi hizo : ............ na .........

Nasoma herufi, matamko, maneno na misemwa.

W h s y f z ngw ch nz W H S Y F
Z Ngw Ch Nz w h s y f z ngw ch nz
W H S Y F Z Ngw Ch Nz b e u l c
o nd ng mw B E U L C O Nd Ng
Mw b e u l c o nd ng mw B E U L
C O Nd Ng Mw a k d j m i n sh
mb Sh A K M J I N D Mb mb j k
d m i a n sh I A M D J K Sh Mb

he wa si fi nzi yu za ngwi

Zamani hewa fizi wazi canjo fundi ziwa
sifa cungwa tafazali

Nzonzi anakula cungwa.
Mtoto anapata canjo.
Mwanafunzi anaenda somoni.
Feza anaenda kwenye ziwa.

Naongeza neno katika msemwa huu.

Feza anaenda sokoni.

Feza anaenda...........

# Juma ya 4

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :




Nacora ceti kimoja ca elimu.

## Nasoma herufi.

g p t r v ny lw kw mbw
G P T R V Ny Lw Kw Mbw
g p t r v ny lw kw mbw
G P T R V Ny Lw Kw Mbw

## Natunga matamko.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| m | o | c | mw | ng | l | nz | p | ny |
| nd | sh | u | e | k | a | ch | t | lw |
| b | d | n | j | mb | i | ngw | r | kw |
| w | h | s | y | f | z | g | v | mbw |

nya
.............
.............
.............

## Natunga maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ra | nyi | mbwa |
| pa | mbo | vi |
| lwa | vu | ngi |

imbwa
....................
....................
....................

## Natunga misemwa.

| | | |
|---|---|---|
| naona | rangi | Vumilia |
| nyumba | panya | ina |
| kwako | imbwa | |

Vumilia, naona imbwa.
......................................
......................................

Natazama.



Nasoma.

## Sherehe

Lwango na Tambwe wanamaliza cuo kikuu.
Wanapata vyeti vyao na alama nyingi.
Wanavaa taji la maua kicwani.
Kweli wanapongenzwa na watu wote.
Habari hiyo inatangazwa katika gazeti.

Katika neno « baraka », nabadirisha tamko « ba » na tamko nyingine na natengeneza msemwa huu.

..... raka

Kicwani la maua taji wanavaa.

..........................................

## Nasoma herufi, matamko, maneno na misemwa.

g p t r v ny lw kw mbw G P T R V
Ny Lw Kw Mbw *g p t r v ny lw kw mbw*
*G P T R V Ny Lw Kw Mbw* W h s y
f z ngw ch nz W H S Y F Z Ngw Ch
Nz *w h s y f z ngw ch nz W H S Y F Z*
*Ngw Ch Nz* b e u l c o nd ng mw B E
U L C O Nd Ng Mw *b e u l c o nd ng*
*mw B E U L C O Nd Ng Mw* a k d
j m i n sh mb Sh A K M J I N D
Mb *mb j k d m i a n sh I A M D J*
*K Sh Mb*

ga pi to ro vu lwi mbwi kwa

gari vuka piga kwetu mbwa raha gari
tajiri kwako kazi

Karibu kwetu.
Fatu anapata ceti ca elimu.
Nyumba yao ina rangi nyeupe.
Safi anavaa kanzu ya rangi nyeusi.

## Natengeneza msemwa huu.

vyeti wanapata nyingi vyao na alama.

.............................................................

# Juma ya 5

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika kanuni tatu za afya nilizosikia.

1.

2.

3.

Natazama.



Nasoma.

## Kanuni za afya

Mama anamukumbusha Dani kanuni za afya. Kanuni zilitolewa na mama Ramina.

Dani, fua mavazi mbele ya kuyavaa. Nawa mikono na sabuni ao majifu. Dani, usilale na mbuzi katika cumba. Unapo amuka, fungua dirisha ya cumba. Fagia na koropa cumba, fua shuka zako.

Dani anahaidi kutimiza kanuni za afya. Kwa hiyo wazazi wake wanafurahi.

Naandika kanuni mbili za afya ninazojua.

Najaza misemwa hii na majina haya: cumba, kijiji, wazi, mbuzi.

1. Dirisha ya ......................... ca Dani

ni .......................

2. Usilale na ..............katika.............cako.

Andika majina matatu ya watu, nyama na vitu.


| Watu | Nyama | Vitu |
|---|---|---|
| 1. | 1. | 1. |
| 2. | 2. | 2. |
| 3. | 3. | 3. |

Naandika  nyama tano sipashwi kulala nazo katika cumba.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |
| 4. |
| 5. |

Naandika misemwa miwili kuhusu usafi wa mwili, nguo na cumba.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.




Naandika vitu viwili mama yako anafanya nikingonjwa.

1.

2.

Natazama.



Nasoma.

Mganga somoni

Leo mama mganga alifika somoni. Kiongozi alimtembeza katika ma darasa zote. Nyumbani, Fatu anaongelea wazazi mashauri ya mama mganga: Mulale cini ya candarua, muoshe mikono na sabuni.

Dani naye anasema mashauri za mama mganga aliwapatia : Musukue meno na mswaki na  musiceze katika mucanga.Kweli ! Watoto wanapata mafundisho bora somoni.

Naandika mashauri matatu ya afya ninayotimiza nyumbani kwetu.

Katika majina haya, natia mzunguko ku majina za pekee na napiga kistari ku majina za jamii :

Dani, wazazi, afya, cumba, Ramina, kanisa, mama, bahati.

Naandika misemwa miwili inayokuwa na majina za pekee na misemwa miwili inayokuwa na majina za jamii.

Misemwa na majina za pekee:

| |
|---|
| 1. |
| 2. |

Misemwa na majina za jamii:

| |
|---|
| 1. |
| 2. |

Naandika  wafanyakazi watatu wa kituo ca afya wanaweza fanya matembezi somoni.


| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu matunzo katika vituo vya afya.

KIPINDI CA PILI

# KUKINGA MAZINGIRA

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika aina tatu za cakula ninacokula zaidi.

1.

2.

3.

Natazama.



Nasoma.

Wakati wa kula

Wakati wa kula unatimiya, mama anatayarisha meza. Mezani, anatia : wali, muhogo, ugali, nyama za mifupa, sombe, mayayi, viyazi, maziwa, matunda, maji na jusi.

Tuna alikwa mezani ; baba, mdogo wangu na mimi. Kila mtu anakamata cakula  kwa utaratibu.

Mdogo wangu anatafuna mfupa. Bahati mbaya, anajivunja jino. Hakika nyumbani kwetu twakula cakula timilifu.

Naandika majina mbalimbali ya cakula.

Kwa kila jambo, naandika jina moja kwa umoja na naitia kwa uwingi :


| | |
|---|---|
| M/wa : | Mama |
| | Wamama |
| M/mi : | 1........... |
| | 2. .......... |
| Ji/me : | 1........... |
| | 2. .......... |
| Ji/ma : | 1........... |
| | 2. .......... |

Naandika  aina tatu za cakula.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu vyakula viwili ninavyopenda kula.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika matunda matatu ninazokula zaidi.

1.
2.
3.

Natatazama.



Nasoma.

Njiani

Safi na wenzake wanatoka ku masomo mcana kati. Wana kiu saana. Wanaona duka cini ya mti wa embe. Dukani wanauzishi jusi ya matunda , maji na ndazi tu.

Mtumishi anakaribisha Safi na wenzake kukaa kwenye viti. Anawapa vikombe vya kujaa jusi ya matunda ya baridi. Mtumishi anavitia kunako meza inayo funikwa na nguo nzuri. Safi na wenzake wanafarijika na wanarudi nyumbani.

Naandika jusi ya tunda naweza kunywa wakati nina kiu.

Kwa kila jambo, naandika jina moja kwa umoja na naitia kwa uwingi :

| N/n : | Nguo |
|---|---|
| | Nguo |

| M/m: | 1. ................................ |
|---|---|
| | 2. ................................ |

| Ki/vi : | 1. ................................ |
|---|---|
| | 2. ................................ |

Naandika matunda matatu napenda kula.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu jusi ya matunda ninayotumia baada ya kula.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za matunda tunazovuna katika pori ya kwenu.

1.
2.
3.

Natazama.



Nasoma.

## Matembezi porini

Wakati wa mafungo makubwa ni wakati wa matunda mwituni. Siku ya posho alarasi ni siku ya matembezi porini.

Watoto wanawake na wanaume wanacimba matunguu pori na vihama. Wanacuma mulenda kwa sababu ni mboga. Tena mulenda unamaliza ugonjwa wa moyo.

Nyumbani, mama anapika mulenda, samaki na ugali. Pori inatutolea cakula, ndiyo maana tunaikinga. Tukirudi somoni, tutaandika ku ubao jina  za matunda na mbonga.

Naandika tunda inayopatikana katika pori za kwetu.

Natia kwa uwingi misemwa hii :

1. Mwimbaji anavaa taji la ua.

..................................................

2. Washi wanajenga ulalo.

..................................................

3. Ulimi una rangi nyekundu.

..................................................

4. Ungo wa mguu.

..................................................

5. Dani anavaa udara.

..................................................

Nacagua neno isiyofanyika wakati wa mafungo makubwa.

| |
|---|
| Kucuma |
| Kupanda |
| Kulima |
| kuenda darasani |
| Shamba |

Naandika misemwa miwili kuhusu mavuno.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika fasi tatu ambapo nimekwisha panda miti.

1.
2.
3.

Natazama.




Nasoma.

## Tukinge mazingira

Miti za Kongo ni mali na utajiri wa Kongo. Kongo ya mashariki na ya katikati kuna miti mingi na mvua ni mingi mahali hapo. Miti inatuletea mvua, inaepusha jangwa na mito zetu zinajazwa na maji. Tusikate miti, bure tutaharibu inci zetu na kugeuka jangwa.

Imekatazwa kabisa kwenye serkali kukata miti bila ruhusa. Ukikata miti bila ruhusa, utalipishwa faini. Uki ruhusiwa kukata mti, utaombwa upande ingine. Tukinge mazingira yetu. Miti inatuletea ubaridi na hewa nzuri.

Naandika ninacofanya kwa kukinga mazingira.

Naandika misemwa tano ya kuhakikiisha :

1. ........................................................................................

2. ........................................................................................

3. ........................................................................................

4. ........................................................................................


5. ........................................................................................

Nacagua vitendo vinavyoweza kunileta malipizi.

| |
|---|
| Kukata miti |
| Kukinga mazingira |
| kulunguza pori |
| Kuotesha majani |
| Kutupa uchafu mtoni |

Naandika misemwa miwili kuhusu vitendo ninavyofanya kwa kukinga mazingira.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za nyama za ufugo ninazopenda.

1.
2.
3.

Natazama.



Nasoma.

Kuku na mbuzi

Zamani za kale, jamaa moja ilifuga kuku na mbuzi. Mbuzi alikua nalala nje katika kibanda, kuku nyumbani.

Alipofika mgeni usiki kati ; sasa, atakula nini ? Akatolewa sombe. Kesho atakula mbuzi, ginsi mama wa nyumba alimuaga.

Kuku alisikia habari hio na akamcekelea mbuzi asubui. Wakati wakumcinja mbuzi wakamuona na mimba. Kwa uepesi wakahamua kumcinja kuku. Usicekelee mwenzako kwa uepesi, haujui ifatayo.

Naandika jina moja la nyama tunafuga nyumbani kwetu.

Nageuza misemwa hii katika maulizo :

1. Mbuzi alikua nalala inje.

..........................................................................

2. Mgeni alifika usiku kati.

..........................................................................

3. Kesho mgeni atakula mbuzi.

..........................................................................

4. Kuku alisikia habari hiyo.

..........................................................................

5. Mama wa nyumba alimuaga mgeni.


..........................................................................

Naandika  maulizo matatu kuhusu ufugo.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu tabia ya kuku katika hadisi « kuku na mbuzi ».

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za nyama za mwitu.

1.

2.

3.

Natazama.



Nasoma.

## Ndoa ya ngamia

Ngamia atalunga ndoa leo ! Anavaa kama mtoto wa mfalme akimcunga mcumba wake. Anatembeya na kujibonja, lakini hamuoni mcumba wake. Anajisemea : hayakuja bado ! Hawezi gawia tena ! Ngamia ananyoosha shingo akiita mcumba :
« Sinifu ! Sinifu ! Kuja ! ».

Nyama zote zinamusikia, lakini, zinamuzarahu. Ngamia anajiona mrembo, hawatilie nyama fitina. Ngamia ana kitumaini tu : mcumba wake atafika. Ah ! Uje, mcumba wangu ! nitakucunga tena kesho !

Naandika nyama moja inayopatikana porini kwetu.

Nafanya misemwa hii ionyeshe hali ya sikitiko ao ya furaha :

1. Gamia atalunga ndoa leo.

..........................................................................

2. Lakini, hamuoni mcumba wake.

..........................................................................

3. Nyama zote zinamuzarahu.

..........................................................................

4. Ngamia ana kitumaini tu.

..........................................................................

5. Nitakucunga tena kesho.

..........................................................................

Naandika  misemwa mitatu yakuonyesha hali ya furaha ao sikitiko.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kwa kuonyesha hali ya ngamia siku ya ndoa yake.

KIPINDI CA TATU

# KUENDELESHA JIMBO MBELE

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za kazi kizazi cangu kinafanya tokea mababu zangu.

1.
2.
3.

Natazama.



Nasoma.

## Mavuno

Mwana Nsapu, mulimaji muhodari , ana umri wa miaka makumi saba. Vijana wa kijiji wanazoea kumuita tu ; kambo Mwana Nsapu. Ana shamba lake la mihogo, mihindi, maboga, mahalagi na viazi.

Wakati wa mavuno, Mwana Nsapu hapendi vijana wabaki wazembe. Anawaomba vijana wamusaidie : Eh vijana ! Munisaidie ili kesho muwe wafanyakazi wahodari.

Kila siku ya mavuno, Mwana Nsapu anapatia kila kijana nusu ya mavuno. Kijiji kizima kina furaha wakati wa mavuno ku shamba la  Mwana Nsapu.

Naandika kazi ya shamba ninapenda kufanya kijijini kwangu.

Angalia msemwa huu :

Mwana Nsapu analima shamba.

Ninatia msemwa huu katika hali ya kukana :

Mwana Nsapu hakulima shamba.

Sasa, natia misemwa hii katika hali ya kukana :

1. Mwana Nsapu, mulimaji muhodari.

   ..............................................................

2. Anashamba lake la mihogo.

   ..............................................................

3. Anaomba vijana wamusaidiye.

   ..............................................................

4. Ana umri wa miaka makumi saba.

   ..............................................................

5. Kesho muwe wafanyakazi wahodari.

   ..............................................................

Naandika miezi mitatu ya furaha katika mwaka.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu kazi ya shamba.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika kazi mbili za ufundi wazazi wangu wanafanya.

1.

2.

3.

Natazama.



Nasoma.

## Kutengeneza johari

Mama Mulenga anafundisha vijana ginsi ya kutengeneza johari : Munapo kuwa katika kiwanda kwa kutengeneza johari, mutokoshe cungu ya madini ya shaba. Mucukue madini ya shaba safi na muyapoleze, mutumie vyombo kama nyundo na koleo.

Mukifanya hivyo, mutatengeneza johari nzuri saana. Vijana wanasikia mafundisho na wanaahidi kuyatimiza.

Naandika mashauri ya zaidi ningependa mama Mulenga anitolee.

Angalia msemwa huu :

Mama Mulenga anafundisha vijana ginsi ya kutengeneza johari.

Ninatafuta mwenyi wa tendo katika msemwa huu :

Nani ana fundisha vijana ? (Mama Mulenga)

Sasa, natafuta mwenyi wa tendo katika misemwa hii :

1. Vijana wanacukua madini ya shaba.

   Mwenyi wa tendo ni:...................................................

2. Tulitengeneza johari nzuri sana.

   Mwenyi wa tendo ni :..................................................

3. Mama Mulenga anapana mafundisho.

   Mwenyi wa tendo ni :..................................................

4. Wanatumia nyundo na koleo.

   Mwenyi wa tendo ni :..................................................

5. Mama Mulenga anauzisha johari sokoni.

   Mwenyi wa tendo ni :..................................................

Naandika mashauri matatu napenda wanitolee.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu kazi mbalimbali ya mikono.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za viongozi wa kijiji cangu.

1.

2.

3.

Natazama.



Nasoma.

## Tushiriki kwa uongozi wa mtaa

Wazazi wa Fatu wanaongelea jirani uongozi wa mtaa walio zungumziwa na mkuu wa mtaa : Jirani, uongozi wa mtaa wetu una ofisi nyingi. Kila ofisi  inatumika kwa maendeleo ya mtaa wetu.

Kila wakati tukizaa, tuandikishe watoto ku serkali ili : Wawe na jina, uraia na  wajue wazazi wao, wawe na haki ya kupata matunzo, canjo na kushiriki ku ucaguzi, wasilazimishwe kuolewa ao kuandikwa katika jeshi kabla ya umri.

Tukifanya hivyo, tutacangia kwa uongozi wa mtaa wetu.

Naandika majina za ofisi mbalimbali za uongozi wa mtaa wangu.

Angalia msemwa huu :

Kila wakati tukizaa, tuandikishe watoto ku serkali.

Ninatafuta timizo la tendo katika msemwa huu :

Kila wakati tukizaa, tuandikishe nani ? (Watoto)

Sasa, natafuta timizo la tendo katika misemwa hii :

1. Baba anauzisha nyama za ufugo.

   Timizo la tendo ni : ..................................................

2. Tuandikishe watoto ku serkali.

   Timizo la tendo ni : ..................................................

3. Mama ana shamba la mihogo.

   Timizo la tendo ni : ..................................................

4. Watoto wote wana haki ya kupata matunzo.

   Timizo la tendo ni : ..................................................

5. Kijiji cangu kina njia nyingi.


   Timizo la tendo ni : ..................................................

Naandika ofisi tatu zinazo unda uongozi wa kijiji cangu.

| | |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |

Naandika misemwa miwili kuhusu uongozi wa kijiji.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.




Naandika aina mbili za usafiri ninatumikiisha kwa kuenda somoni.

1.

2.

Natazama.



Nasoma.

Njia za kijiji

Kijiji cetu ni wazi, tunatembea bila shaka. Wakati wa mavuno, njia ndogo zatusaidia kwenda shambani. Zatusaidia pia siku ya soko kwenda katika vijiji jirani.

Tunasafiri juu ya jito na mtumbwi wa mkuu wa kijiji. Mtumbwi yasaidia kwa kuvukiisha biashara na mavuno ya wakaaji wote.

Ila ni vigumu kuona gari kwa sababu hakuna barabara. Tunapendelea kijiji cetu kiwe na barabara kubwa ili kifunguke zaidi.

Naandika njia mbalimbali ninatumia kijijini kwangu.

Angalia msemwa huu :

Mtumbwi unatusaidia kwa  kuvukiisha biashara.

Ninatafuta timizo la tendo katika msemwa huu :

Mtumbwi unatusaidia kwa nini ?( kuvukiisha biashara)

Sasa, natafuta timizo la tendo katika misemwa hii :

1. Mganga anatumia darubini.

   Timizo la tendo  ni :.................................................

2. Watoto wanazungumuza na wazazi wao.

   Timizo la tendo  ni : .................................................

3. Waalikwa wanahuzuria karamu ya ndoa.

   Timizo la tendo  ni : .................................................

4. Tulisafiri na basi kubwa.

   Timizo la tendo  ni : .................................................

5. Wanafunzi waandika na kalamu ya risasi.


   Timizo la tendo  ni : .................................................

Naandika njia tatu za usafiri wakaaji wanatumia kijijini.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu usafiri kijijini.


Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora kinga.



Natazama.



Nasoma.

Maendeleo ya kijiji

Mangaribi kiisha kikao ca vijana, Cansa anarudi nyumbani kwao. Anaongelea  ndugu zake kuhusu mradi wao wa maendeleo. Anawaelezea yakwamba, barabara ziki jengwa : Wababa wataenda shambani kwa kinga, watoto wataenda ku masomo na mahali pengine kwa pikipiki.

Gari kubwa na ndogo, zitaleta wacuuzi katika Kijiji. Hapo, mavuno na biashara mbalimbali vitauzwa. Kijiji cao kitasonga mbele.

Naandika vyombo  mbalimbali vya usafiri  nitatumia maendeleo ikiwa kijijini kwangu.

Angalia msemwa huu : Mangaribi, Cansa anarudi nyumbani kwao.

Natafuta timizo la wakati : Cansa anarudi wakati gani ?

Timizo la wakati ni : Mangaribi.

Natafuta timizo la mahali : Cansa anarudi wapi ?

Timizo la mahali ni : Nyumbani kwao.

Sasa, natafuta timizo la wakati na lile la mahali katika misemwa hii :

1. Asubui mapema, tate anaenda shambani.
   Timizo la wakati ni : ..........................
   Timizo la mahali ni : ........................................

2. Kila mwaka vijana wanafanya matembezi porini.
   Timizo la wakati ni : ........................
   Timizo la mahali ni : ........................................

3. Tunaceza kabumbu kiwanjani siku ya posho.
   Timizo la wakati ni : ..........................
   Timizo la mahali ni : ........................................

Naandika vyombo vitatu vya usafiri.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu yombo tunacukua kwa usafiri kijijini kwetu.

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora gari la mabawa uwanjani.

Natazama.



Nasoma.

Napenda kusafiri

Napenda kusafiri kwa sababu najifunza vitu vingi katika safari. Safari yatujulisha migini mbali mbali, watu, pori, bahari, tabia ya mahali. Hasa safari ya gari la mabawa katika anga na pepo.

Ndani ya gari la mabawa naona rubani, wabinti na wavulana wanaosaidia wasafiri. Mbele ya gari la mabawa kuruka, inatembea cini na duara zake za kidogo. Wakati gari la mabawa inaruka ao inashuka, wasafiri wanampigia rubani mikono.

Safari ya gari la mabawa ni nyepesi zaidi kushinda masafari zote lakini bei ya safari ya gari la mabawa ni kali.

Naandika nitakacofanya nikiwa ndani ya gari la mabawa wakati inaruka wala inashuka.

Angalia msemwa huu : Napenda kusafiri.
Naongeza sababu gani napenda kusafiri :
Napenda kusafiri kwa sababu najifunza vitu vingi.

Naongeza shabaa ninayopata katika safari :
Napenda kusafiri kwa ajili niwe mwenyi akili.

Sasa, naongeza timizo la sababu ao la shabaa katika misemwa hii :

1. Napenda kujifunza kwa sababu ..............................................................

2. Mama anakaribisha jamaa mezani kwa ajili..................................................................

3. Firimbi la gari la moshi inapigwa kwa sababu..............................................................

4. Vijana hawabaki wazembe wakati wa mafungo kwa sababu..............................................................


5. Dani anafungua madirisha kwa ajili..................................................................

Naandika vitendo vitatu nitafanya nikiwa ndani ya gari la mabawa wakati inaruka ao inashuka.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa miwili kuhusu usafiri wa gari la mabawa.

Naelezea wandugu wangu hadisi hii.



Naandika majina matatu za micezo za kiasili ninazojua.

1.
2.
3.

Natazama.



Nasoma.

## Mashindano ya micezo

Leo, timu mbili zitashindana kuhusu kange katika uwanja wa mtaa.

Timu Ujana ina mabinti warembo, warefu na wahodari. Timu Ukweli ina mabinti warembo pia, wafupi na wa nguvu tele.

Mwamuzi wa kijiji kingine alifika kuongoza mashindano hayo. Mwamuzi anapiga firimbi ya mwanzo. Binti moja wa timu Ukweli anaanzisha mcezo. Mashindano iko nguvu, watu wanalalamika kwa kujuhudisha matimu. Kiisha dakika makumi mane : timu Ujana linawina.

Naandika mcezo miwili ya kiasili napenda kuceza.

Angalia neno hii :

Kanzu ........................................................

Naongeza elezo la hali mpebeni ya jina kanzu :

Kanzu mrefu.

Sasa, naongeza maelezo za hali ku nafasi ya wazi pembeni na jina hizi :

1. Mwalimu ..................................................

2. Mzazi ......................................................

3. Muhuguzi ................................................

4. Muimaji ...................................................

5. Mvulana ..................................................

Naandika micezo mitano za kiasili.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |
| 4. |
| 5. |

Naandika misemwa mitatu kuhusu micezo za kiasili.

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :




Nacora kabumbu.

Natazama.



Nasoma.

Mapambano

Mimi na wazazi wangu tunaishi katika mji mkuu. Marafiki wangu na mimi tunapenda sana kufanya mazoezi kila siku ya ine somoni. Kila siku ya posho, tunahuzuria zaidi mcezo wa kambubu ku uwanja wa mtaa.

Siku ya posho hii tutaenda kijijini kwa babu kutazama mcezo wa kugombana. Vijana wawili wa umri wa  miaka kumi na sita watagombana pale. Mwenye atatua mwezake cini wa kwanza anapata ushindi.

Mcezo huu wa kugombana si wa ma adui wala wa cuki. Ni mazoezi tu, kwa kuleta nguvu ya mwili.

Naandika mcezo wa mazoezi napenda ili kuleta nguvu mwilini.

Angalia misemwa hii, vielezo vinapigwa kistari :

Marafiki wangu na mimi tunapenda <u>sana</u> kufanya mazoezi, <u>hivyo</u>, siku ya posho tutaenda kijijini.

Sasa, katika misemwa hii, natafuta vielezo na napiga kistari cini :

1. Napenda sana kula vitika.

5. Njiani tunaongea kuhusu ushindi.

4. Watazamaji pia wanarukaruka.

3. Baba hakusema hivyo.

2. Wadogo wangu wanasema hivi.

Naandika micezo mitatu ya kikundi.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa mitatu kuhusu micezo za kikundi.

Natazama kiisha naeleza hadisi hii :



Nacora mtu anakimbia mbio.

Natazama.



Nasoma.

Mcezo wa loko

Dani na Fatu wanaceza kila mara wakimaliza mapashwa yao ya masomo.

Leo wanahamua kuceza mcezo wa loko. Dani anacora loko udongoni pale nyuma ya nyumba yao, anamuita Fatu waceze mbele waende kula cakula ya mangaribi.

Fatu anaceza mtu wa kwanza, lakini, anafinyanga mustari. Ni zamu ya Dani sasa ; anasukuma jiwe kwa rafla. Anaruka haraka manyumba ya loko bila kosa. Dani anafunga nyumba ya pili.

Naandika mcezo naceza nikimaliza mapashwa ya masomo.

Angalia misemwa hii, vielezo vinapigwa kistari :

- Leo, mcezo wetu ulikuza mzuri.
- Tuliceza bila shaka.

Sasa, katika misemwa hii, natafuta vielezo na napiga kistari cini :

1. Nyuma ya masomo yetu kuna uwanja.

1. Dani anasukuma jiwe lake mbele.

2. Hakika, Fatu anafunga nyumba ya pili.

3. Kesho tutaceza mcezo wa kabumbu.

4. Bado mwamuzi hajapiga firimbi.

Naandika  micezo mitatu za kipekee.

| |
|---|
| 1. |
| 2. |
| 3. |

Naandika misemwa mitatu kuhusu micezo za kipekee.

Ce cahier de lecture a été imprimé grâce à l'appui généreux du peuple américain et du peuple britannique, à travers l'Agence des Etats-Unis pour le Développement International (USAID) et le Ministère Britannique de la Coopération Internationale (DFID/UKAID).

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people